# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI KABITA
S.L.P 40,
**BUSEGA.**

**KUMB. Na.KSS/S.1595/…….** 15/12/2020

Jina la Mwanafunzi ……

Shule ya msingi unayotoka…….

Busega.

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KABITA WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021</u>**

**1.0. UTANGULIZI**

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Kabita ni ya kutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (Wavulana na Wasichana). Ipo umbali wa kilometa 4 kutoka Nyamikoma katika kijiji cha Kabita kandokando ya ziwa Viktoria. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku kumi na nne

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1. Sare ya shule:

i. **Wavulana:** Suruali damu ya mzee (namba 1) mbili zenye marinda mawili kila upande, mkunjo wa chini “turnup” mzingo kwa chini inchi 21.

ii. **Wasichana :** Sketi damu ya mzee (namba 1) mbili rinda boksi, beriti isizidi ichi mbili ndefu

iii. Mashati meupe mawili mikono mifupi yawekwe alama ya kidato bega la kushoto kwa kutumia rangi ya kitambaa cha suruali/sketi.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi.

v. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo mapambo kwa wasichana, nyeusi kwa wavulana.

vi. Viatu vya Ngozi vyeusi vyenye kamba na T-shirt ya bluu kwa ajili ya michezo na sweta rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya baridi.

vii. **KWA WANAOVAA HIJAB.** Mashono ya nguo yazingatie maadili ya dini husika.

viii. Tai sawa na sketi na suruali (damu ya mzee).

**NB: Ni muhimu kufuata maelekezo katika ushonaji wa sare za shule na siyo vinginevyo.**

2.2 Vifaa vya kujifunzia: Daftari kubwa 12, kalamu, rula na mkebe wa hesabu (Mathematical set).

2.3 Dictionary (Kamusi ya Kiingereza)

**2.4 VIFAA VYA USAFI**

Mfagio wa chelewa na ndoo kwa ajili ya kumwagilia maua na miti kwa WASICHANA, Jembe lenye mpini kwa WAVULANA**.**

**3.0.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,sayansi na tekinolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

a) Mahuzurio mazuri kila shughuli ndani ya nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
b) Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h) Kutunza mali za umma.

**1.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.

k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

m) Kuwa na simu ya mkononi.

**1.0 MAMBOMENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. **KIAMBATISHO "B"**

b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. **KIAMBATISHO"A"**

c) Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

……

**MARCO JOSEPH HALALI**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI KABITA**

**KIAMBATANISHO "A"**

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**SHULE YA SEKONDARI KABITA**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi _____
2. Shule ya Msingi aliyosoma _____
3. Tarehe ya kuzaliwa _____Kabila _____
   Wilaya _____ Mkoa_____
4. Dhehebu/Dini _____
5. Jina la baba _____
6. Jina la mama _____
7. Unatoka kijiji cha _____Kitongoji cha _____
8. Kazi ya baba _____ kazi ya mama _____
9. Unaishi na wazazi/walezi? Ndiyo / Hapana ***(futa isiyohusika)***
10. Taja Jina kamili la mzazi/mlezi _____
11. Andika namba za simu za mama _____ baba _____ au mlezi _____
12. Cheti cha kuzaliwa namba _____ ***(Njoo na nakala (copy) shuleni)***

**AHADI YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE IKIWA NI PAMOJA NA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi _____ (Jina la mzazi/mlezi) ambaye ni mzazi/mlezi wa _____ (Jina la mwanafunzi)

Nimesoma na kuelewa vyema maelekezo ya mwanagu kuhusu kujiunga na shule ya sekondari Kabita. Hivyo nakubali kuwa nitasimamia kwa ukaribu zaidi malezi na maendeleo ya mwanangu kitaaluma na kinidhamu ili asishiriki kwa namna yoyote ile katika migomo ili aweze kuhitimu Elimu ya sekondari vizuri bila kukwama/kukatisha masomo.

**"KILA MMOJA ATIMIZE WAJIBU WAKE"**

Jina la Mzazi/Mlezi _____

Saini ya Mzazi/Mlezi _____

Namba za simu _____

Tarehe _____

THE HEADMASTER
KABITA SEC. SCHOOL
BUSEGA SIMIYU

**KIAMBATANISHO "B"**
GOVERNMENT OF TANZANIA
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS**
KABITA SECONDARY SCHOOL
**PART A:**

Full Name _____
Age (years) _____height (cm) _____ sex _____ weight (Kg) _____
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for Joining Secondary School. The examination should include the following categories (I - III) each category or sub category of which will render the applicant ineligible in each of a defect. Pregnancy (Plano test), category IV will render a girl student ineligible.

I.
(a) Eye –sight _____
(b) Hearing _____
(c) Speech _____
(d) Venereal disease (HIV) _____
(e) Leprosy and T.B Disease _____
(f) Epilepsy _____
(g) Spleen _____
(h) Chest/Abdomen _____
(i) Blood coat _____ (red/white)
(j) Urinalysis _____

II. Neuroses

III. Additional information e.g Physical defect or impairments, infections, chronic or family/heritable diseases (e.g sickle cell) inability to eat certain food etc. _____
_____
_____

IV. Pregnancy _____

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by Government Medical Officer)**

I have examined the above named school student and consider that he/she is physically and mentally fit/ unfit to take secondary Education course.

Name and Signature _____
Designation _____
Station _____

***(Official stamp)***

THE HEADMASTER
KABITA SEC. SCHOOL
BUSEGA SIMIYU